

## JINSI YA KUTENGENEZA BUSTANI NDOGO NYUMBANI KWAKO



### VIFAA/MAHITAJI

**Udongo, Kokoto (mawe madogomadogo), Gunia, mchanga/Pumba za mpunga (Rice husk), Mbole ya samadi iliooza vizuri, mti/mbao na kopo dogo (sadolini).**

### MATUMIZI YA VIFAA

**Udongo** - Kwa ajili ya kuwezesha mmea kusimama, pia kupatia virutubisho mmea

**Mchanga/Rice husk** - Kusaidia mizizi kupita kwa urahisi, pia kuweka mazingira mazuri ya hewa na maji katika udongo yaani mzunguko wa maji na hewa.

**Kokoto** - Kusaidia maji kupita ndani ya gunia toka juu hadi chini

**Mbolea ya samadi** - Kutoa virutubisho kwa mmea  
**mti/Mbao** - Kusaidia gunia lako kusimama vyema/ imara



## MATUMIZI YA VIFAA

**Udongo** - Kwa ajili ya kuwezesha mmea kusimama, pia kupatia virutubisho mmea  
**Mchanga/Rice husk** - Kusaidia mizizi kupita kwa urahisi, pia kuweka mazingira mazuri ya hewa na maji katika udongo yaani mzunguko wa maji na hewa.

**Kokoto** - Kusaidia maji kupita ndani ya gunia toka juu hadi chini

**Mbolea ya samadi** - Kutoa virutubisho kwa mmea

**mti/Mbao** - Kusaidia gunia lako kusimama vyema/ imara

## HATUA ZA UTENGENEZAJI.

(i) Changanya udongo wako na mchanga/rice husk pamoja na mbole katika uwiano wa 5:2:1. Ndoo 5 udongo, 2 samadi, 1 Mchanga/rice husk.

(ii) Toboa kopo lako na ondoa kitako ili kuweka uwazi pande zote mbili (juu na chini)

(iii) Weka mti/ubao katikati ya gunia ukiuchimbua ardhini kisha weka kopo lako katikati ya mti/mbao hiyo na lijaze kokoto

(iv) Weka udongo uliochanganywa vizuri kwenye gunia lako ukilizunguka kopo lenye kokoto hadi kufikia kimo cha kopo. Baada ya hapo ondoa kopo na hakikisha kokoto zinabaki zikizungukwa na udongo.

(v) Weka kopo juu ya kokoto zilozungukwa na udongo kisha, lijaze kopo hilo na kokoto, rudia kujaza udongo ukilizunguka kopo hadi kimo cha kopo hilo. Endelea kufanya hivyo (kama hapo juu) hadi pale gunia lako litakapokuwa limejaa.

(vi) Toboa gunia kwa kuweka matundu kuzunguka gunia kwa ajili ya kupandia katika umbali sawa (inategemea na aina ya mboga)

## KILIMO CHA BUSTANI KWENYE KIROBA



NANENANE 2017

**KWA TAARIFA  
ZAIKI TEMBELEA  
TOVUTI YETU**

[www.masasidc.go.tz](http://www.masasidc.go.tz)

[infor@masasidc.go.tz](mailto:infor@masasidc.go.tz)